# MASWALI YA KCSE YA FASIHI SIMULIZI

## MAJIBU 140 KWA 0707311302 au Rejelea majibu ya mitihani ya KCSE.

## 2007-2019

**2007- Lazima-ushairi**

(a) Nini maana ya mighani/migani? (alama 4)

(b) Fafanua sifa za mighani/migani. (alama 10)

(c) Eleza umuhimu wa mighani/migani. (alama 6)

**2008- Lazima-Ushairi**

Fafanua sifa zozote kumi za mtambaji bora wa ngano. (20 alama)

**2009-Lazima-Riwaya**

a) Ni nini maana ya mawaidha? 2

b) Huku ukitoa mifano mwafaka, fafanua muundo wa mawaidha katika fasihi simulizi. 4

c) Eleza sifa saba za mawaidha katika fasihi simulizi. 14

**2010-lazima-Ushairi**

Huku ukitoa mifano mwafaka, **linganisha** na **utofautishe** kipera cha vitendawili na kile cha methali.

**2011-lazima, Tamthilia**

. (a) Eleza maana ya malumbano ya utani.(alama 2)

(b) Bainisha sifa **nne** za malumbano ya utani. (alama 8)

(c) Fafanua majukumu **matano** ya malumbano ya utani katika jamii.(alama 10)

**2012-lazima, Hadithi Fupi**

(a) Huku ukitoa mifano, fafanua majukumu matano ya nyimbo. (alama 10)

(b) "Mwimbaji ana nafasi muhimu katika kufanikisha uwasilishaji wa wimbo. (alama 10)

**2013-lazima, Fasihi Simulizi**

(a) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya vitanza ndimi. (alama 2)

(b) Fafanua majukumu sita ya vitanza ndimi katika j arnii, (alama 6)

(b)Eleza mbinu sita unazoweza kutumia katika kukusanva na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi (alama 12)

**2014-lazima, Riwaya.**

(a) *Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Basi *Mulungu* akamturna kinyonga duniani kumpasha binadamu ujumbe ufuatao: "Maisha yako hayatakuwa na mwisho, hata ukifa utafufuka."

Kinyonga akaondoka kama mshenga apelekaye posa. Akatambaa polepole, moyoni amejawa na hofu ya kuiharibu ardhi ya wenyewe. Hata alipowafikia binadamu machweo ya siku ya saba baada ya kupashwa ujumbe, alimpata mnana keshaubatilisha ujumbe huo; ameisha kumwambia binadamu kuwa akifa atatokomea kama mizizi ya msubili. Huo ukawa ndio mwanzo wa mauti.

(i) Andika aina ya hadithi hii. (alama 2)
(ii) Fafanua umuhimu wa aina hii ya hadithi katika jamii. (alama 10)
(a) Eleza majukumu **manne** ya fomyula ya kumalizia katika ngano,: (alama 8)

**2015-Lazima, Fasihi Simulizi**
(a) Hadithi ya Jabari inasimuliwa na jamii nyingi. Jabari alizaliwa kashika mkuki mkononi. Mawio ambayo ni kilio chake, ambacho kwa kweli kilikuwa mngurumo, kilipopasua anga, nyota kubwa ilianguka kutoka mbinguni. Ulimwengu ulitetemeka na kutwaa giza.

Hata kabla mama mtu hajampa ziwa, Jabari alikuwa amevuvumka na kuwa gulamu wa miraba mine. Haikuchukua muda, hata vita kati ya jamii ya Sule na SUna vikaanza; kikosi cha Sule cha wapiganaji mia moja kikawajia vijana wa Suna na Sule kwa sime na nyuta. Jabari aliwakabili kwa konde moja pekee, akakirambisha dongo kita kizima.
a. Bainisha kipera cha utungo huu. al.1

b. Toa sababu mbili kuthibitisha jibu lako a hapa juu. al 1

c. Eleza manufaa sita ambayo jamii itapata kwa kurithisha kipera hiki kwa vizazi vijavyo. al. 6

(b) Ndimi mwino mdumishaji ukoo

Ndimi ndovu mtetemesha ardhi
Aliyepigana vita, ikoo kauni
Zilizorindima zangu nyayo
Adui alinywea, mafahali na mitamba akatukabidhi
Kwenye misitu sikuwa na kifani
Paa na hata visungura
Vilijikabidhi kwangu
Kwa kuinusa tu mata
Nani aliyewahi
Ngomani kunipiku?
Makoo hawakunisifu, wakalilia nikaha?
Kwenye Nyanja za michuano
Nani angethubutu, ndaro kunipigia?
Sikuwabwaga chini, kwa yangu maozi, hata kabla hatujavaana.
a) Andika aina ya sifo hii. al.1

b) Bainisha shughuli mbili za kiuchumi na mbili za kijamii zinazoendoelendelezwa na jamii inayosawiriwa na utungo huu. al. 2

c) Eleza mambo matano ambayo yanaweza kuzingatiwa ili kufanikisha utungo uwasilishaji wa utungo huu. al 5

**2016-lazima, Hadithi Fupi.**
(a)Kwa kutumia mifano mwafaka, eleza majukumu ya nyimbo katika jamii. Al 10
(b) Ili kuweza kufanikisha uwasilishaji wa utanzu wa nyimbo kwa hadhira eleza mambo anayohitaji mwimbaji 10
Lazima-kanda la usufi, Shaka ya mambo,Tazamana na mauti

**2017-lazima-wimbo**
Walikuja mahasidi, ah, walikuja
Nyayo zao zikirindima, ah rindima
Kwa ghamidha ya uadui, oo uadui
Wali wakibeba sime
Wali wakibeba mata
Wali wakibeba mienge
Ya moto kutangazia
Kwao kuwasili
Walikuja kwa ndimi
Zilohimili cheche
Matusi kutumwaiya
Hawakujua ya kwamba
Mbele ya mhimili huno wetu
Wao wali vipora
Kwenye mlima wa sugu, walituvamia
Aliwakabili mbwene
Mwana wa ngwamba, ee mbwene
Aliwakabili mbwene kwa kitali kikali
Wali wametuteka ja samaki kwenye dema
Wali wamewapukutisha
Wetu mabarobaro
Aliwakabili mbwene
Ee mbwene, mwana wa ngwamba
Aliwakabili
Kwa hamasa za ujana
Kwa uchungu wa kuumbuliwa
Wa wetu wana.
Aliwakabili mbwene

Nao wakalipiza shambulizi
Kwa kujidai majagina
Walijibwaga uwanjani
Laiti wangalijua wanajikabidhi
Viganjani mwa mbwene
Aliwakabili mbwene, ee
Mwana wa ngwamba, shujaa asoshindwa
Alipigana kitali
Cha kufa na kupona
Kuiopoa jamii yetukuirejesha hadhi yetu
Kuirejesha mifugo yetu
Kuwarejeshea wakulima vikataa vyao
Kuwaokoa vipusa wetu
Nyara waliotekwa, ati walipiza kisasi
Aliwakabili mwana wa ngwamba
Aliwakabili upepo wa kusi
Hata kikomo cha mapambano kilipofika
Wagundi walijua kwamba
Walikuwa na mwana, ee mwana
Mbwene, ee mwana wa ngwamba
Hakuwa na kifani, ee kifani
Alipigana nao, ee mwana wa ngwamba
Kwa siku kumi bila tonge wala tone la maji
Kwetu kukenda kicheko cha wokovu
Kwao kukenda kilio

a) Huu ni wimbo wa sifa. Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano mitatu kutoka kwenye utungo huu. 3

b) Andika sifa tatu za jamii ya nafsi neni katika utungo huu. 3

c) Huku ukitoa mifano, bainisha vipengele vinane vya kimtindo ambapo nafsi neni ametumia kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. 8

d) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii yako. Fafanua hoja sita utakazotumia kuishawishi jamii yako kukinga dhidi ya hali hii. 6

e)

**2018, lazima shairi**

Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.
Nalilitizama jua la kinjano
Likijikokota kwa jitimai kutua
Mbele ya nguu
yam lima uso kikomo

likipisha machweo
yenye giza la kaniki
likishindilia uzito wa nanga
kwenye moyo tepetevu
uloonja shubiri ya kwondokewa
Twalitazama na hiyo shamsi
ikipotelea kwenye upeo wa macho
huku nyuma ikinambia
"yamekwisha."
Naliona kope zake zikimezwa pamwe nawe
Jagina wa maisha yangu.
Nikaliona likikokota aushiyo
Likabwakura rohoyo
Kutoka kwenye vyangu vitanga.
Kumbukizi zilikuleta
kwenye jukwaa la akili yangu
Pazia likafunguka
likayaleta mawio
ya siku ya kuamkia kuuka kwako.
Nalikuona kwenye ruya ukitazamana ana kwa ana
na hasidi alokakawana
kutuhasiri mi nawe
Nalikiona kipaji chako
kikitwaa wasiwasi
ukawa ni kama wanywea
kwa wake mtazamo.
Hata uliponishika
mkono kunambia
tukimbile tujiponye
nalikuwa nimechelewa
ulikuwa keshanipa kisogo, huku
nyuma waniita,
"Mwanangu, njoo tujisalimishe

Mwanangu njoo, nguvu zimenisha."
Kumbe hiyo ilikuwa tahadhari
kwamba iziraili yu karibu
moyowe kuchukua?
Kumbe wali ukisema, "Buriani mwanangu?"
Siku ya faradhi ilifika, mkono kulazimika kukupungia
Naliutazama mwilio mtukufu
Nalilitazama tambolo liloumbuka
wali umedhibitiwa shujaa wangu
ndani ya chumba chenye kuta
na paa la mbao
Hata tulipotukaribisha,
kwa lako kaburi
Nilijipa kujiambia, "Hajenda popote
Mtima bado wapiga."
Nalingoja unisalimu
Nalingojea tabasamu lako lenye haya
Ela hayo hayakutimila
Walikuwa kesha kwenda
Kuwa milki ya ardhi isoshiba
Hata waliponena, "Udongo kwa udongo,"
Nilikusikia ewe yeli uso kifani
Ukighani ubeti wa wimbo
wako pendwa mawazoni mwangu,
"Kifo ni hasidi,
Ikiwa mimi Gunge
Roho yangu nitamkabidhi Iziraili
Mimi niliyekaidi bunduki ya Mzungu
Katika kitali cha miaka minne
Kwetu kukarudi fahari na jina.
Mimi niliyeshindana na ndui na tetekuwanga, iliyowapukutisha
Wana wote wa Ngome
Nikabaki mimi, jogoo wa kijiji.

"Kifo ni shujaa,
Ikiwa mimi Gunge mwili wangu huu mtukufu
Kwa tambo na nemsi
nitaukubalia
kuwa lengo la dua za kuonewa Imani
kuwa karamu ya macho ya mahasimu
kuvikwa suti na mwosha
Kufunikwa kwa udongo uliolaaniwa
Mimi Gunge,
Niliruhusu jabali kubwa
Likibinye changu kichwa
Likidhibiti change kidari
Linizibe zangu pumzi
Gunge niache kutawala."

**Maswali**

a.

i. Huu ni wimbo wa aina gani? al. 1

ii. Andika sababu mbili kuthibitisha jibu lako la a(i). al 1

iii. Ni nani anayeimbiwa na nafsineni? al 1

iv. Bainisha matatizo mawili yanayoikumba jamii inayosawiriwa na utungo huu. al 2

v. Bainisha mbinu zifuatazo katika wimbo huu. al 3

I. Ritifaa

II. Mbinu rejeshi

III. Taashira

vi. Unanuia kutumia mbinu ya kutazama na kushiriki kufanya utafiti kuhusu nyimbo za aina hii. Andika sababu sita za kuchagua mbinu hii. al 6

b. Fafanua mikakati sita ambayo jamii inaweza kutumia ili kuudumisha utanzu wa semi. al 6

**2019, Lazima Riwaya**

**Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.**

Shangazi anambila
Umewadia muda
wa kukiacha kiambo

cha baba
Nende kujinasabisha
na ajinabi tusohusiana
kwa ngeu wala usaha
nache niwapendao
nache aila
nache matamanio
ya elimu kufuatiya
Anambile shangazi
Hino ni neema
ela moyo wanirai
"Wajitia shemere", name nauambia,
"Najua si utashi wangu"
ila hiari sina
kwani hii ni faradhi
mitamba mepokelewa
na ami kwa furaha
kilobaki ni kuvuka
kizingiti hiki."
Kwaheri mama, kwaheri wanuna.

(a) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. al. 2

(b) Andika sifa mbili za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. al. 2

(c) Eleza mikakati sita ambayo mwimbaji angetumia kufanikisha uwasilishaji wa wimbo huu. al. 6

(d) Unanuia kutumia mahojiano kukusanya habari kuhusu nyimbo za aina hii.
i. Eleza manufaa matano ya kutumia mbinu hii. al. 5

ii. Eleza changamoto tano za kutumia mbinu hii. al. 5